# HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI

**(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kigamboni)**

Simu: +255 22-2928468
Fax: +255 22-2928469
Barua pepe: info@kigamboni.go.tz
Tovuti: www.kigamboni.go.tz

S.L.P. 36009,
KIGAMBONI,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

Kumb.Na. LD/TM/VIJ/10889/15/JWM

Tarehe : 08/11/2019

Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
Kanda ya Dar es salaam na Pwani,
S.L.P 9132,
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: KIWANJA NAMBA 935 KITALU '-' VIJIBWENI JIJINI DAR ES SALAAM**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

Tumepokea maombi ya kumilikishwa kiwanja tajwa hapo juu kutoka kwa **ELLAND ROAD LIMITED** katika taratibu za kumpatia makadirio ya kodi za awali Premium kwa mujibu wa makadirio ya mthamini eneo hili limetakiwa kulipia kwa rates za laki moja na nusu (150,000), hivyo Premium ni Tshs. 276,966,562/=.

Hivyo, baada ya kuingiza katika mfumo kiasi cha malipo kinatofautiana na uhalisia wa kiwango cha makadirio yanayotakiwa kulipia.

Tunaomba ofisi yako itusaidie kurekebisha malipo hayo katika mfumo tuweze kumpatia malipo (invoice) kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kumilikisha.

Pamoja na barua hii naambatanisha na nakala ya 'Invoice'

R. A. Mwasha
**Kny; MKURUGENZI WA MANISPAA KIGAMBONI.**

Nakala:

ELLAND ROAD LIMITED,
S L P 50071,
**Dar es salaam.**

Scanned with CamScanner

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

*Simu +255 22 211 3165*
*Nukushi: +255 22 212 4576*
*Barua pepe: cl@ardhi.go.tz*

*1 MTAA WA ARDHI*
*S.L.P 9132,*
*11477 DAR ES SALAAM*

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. LD/348393VOL.III/94**

**16/01/2020**

Mkurugenzi wa Manispaa,
Manispaa ya Kigamboni,
S.L.P. 36009,
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: KIWANJA NA.935 VIJIBWENI.**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Tunakiri kupokea barua yenu ya tarehe 08/11/2019 yenye Kumb.na.LD/TM/VIJ/10889/15/JWM uliyomwandikia Kamishna wa Ardhi Msaidizi Kanda ya Dar es salaam na Pwani. Aidha umesema kwamba mmepokea maombi ya kumilikishwa kiwanja tajwa hapo juu kutoka kwa **ELLAND ROAD LIMITED**, lakini katika utaratibu wa ukadiriaji wa **"Premium"**uliofanywa na Mthamini wa Manispaa kwa kutumia kiwango(land rate per meter square) cha Tsh.150,000/= thamani imekuja Tshs.276,966,562/= ,pia mmesema kuwa baada ya kuingiza katika **mfumo wa Molis** kiasi cha malipo kinatofautiana na uhalisia wa kiwango kilichokadiriwa na mthamini, hivyo mkaomba turekebishe malipo hayo katika mfumo ili muweze kumpatia mteja Ankara (invoice) ya malipo.

Aidha, suala hili lilipelekwa kitengo cha Uthamini ili liweze kufanyiwa kazi, na wamelifanyia kazi kwa kufanya makadirio mapya kwa kutumia kiwango (rate) cha 250,000/= kwa matumizi ya kiwanda. Hivyo basi,tumeambatisha nakala ya makadirio kwa ajili ya marekebisho ya Ankara (invoice).

Pia tunaomba kiwanja hiki kikaguliwe na kuandikiwa ripoti ya uwandani ili kuhakiki kama eneo hili haliingiliani na eneo la upanuzi wa Bandari.

Tunakutakia kazi njema.

E.N.Gari

**Kny : KAMISHNA WA ARDHI KANDA YA DAR ES SALAAM NA PWANI**

Scanned with CamScanner

# HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI

**(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kigamboni)**

Simu: +255 22-2928468
Fax: +255 22-2928469
Barua pepe: info@kigamboni.go.tz
Tovuti: www.kigamboni.go.tz

S.L.P. 36009,
KIGAMBONI,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

Kumb. Na. KGMC/LD/VIJ/10889/20/JWM

Tarehe : 13/05/2020

Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
Kanda ya Dar es salaam na Pwani,
1 Mtaa wa Ardhi,
S L P 9132,
11477 **DAR ES SALAAM.**

**YAH: TAARIFA YA KUWASILISHA HATI ILI ZIPATE SAINI YAKO NA KUSAJILIWA KIWANJA NAMBA 935 KITALU '-' VIJIBWENI JIJINI DAR ES SALAAM**

Tafadhali rejea somo la hapo juu.

Kiwanja tajwa hapo juu kinamilikiwa na **ELLAND ROAD LIMITED** wa S.L.P **50071**, Dar es Salaam. Malipo ya kodi za serikali ikiwa pamoja na ushuru wa serikali yamelipwa kama yalivyoainishwa katika fomu za ushuhuda wa malipo.

Hati ya haki ya kumiliki ardhi yenye **L.O.No. 1048856** imetayarishwa na inawasilishwa kwako kwa saini yako na kisha kwa hatua za usajili pamoja na nyaraka;

i. Nakala ya barua ya toleo 'Allocation Letter'
ii. Nakala halisi ya cheti cha usajili wa Kampuni
iii. Nakala halisi ya Memorandum and Articles of Association
iv. Nakala halisi ya uthibitisho wa uraia wa wakurugenzi wa Kampuni
v. Fomu za uhakiki wa miliki
vi. Nakala ya kiziduo cha "TP Drawing"
vii. Nakala ya mikataba ya mauziano

Taarifa ya kumbukumbu za Ofisi/ Historia: Eneo hili lilikuwa linamiliki na **NOORUDIN ABDALLAH MUSSALLAH** likiwa na viwanja ambavyo havikumilikishwa ni namba 314,315,316,317,318,319 na 320 Kitalu 'A' Kigamboni ndugu, **NOORUDIN ABDALLAH MUSSALLAH** aliuza kwa **Wilmar TZ Holdings Limited** baadae wakatoa viwanja hivi kwa **ELLAND ROAD LIMITED** na kubadilisha mchoro wa ramani na Viwanja hivyo kwa pamoja kusomeka kiwanja namba 935 Vijibweni Light Industry **ELLAND ROAD LIMITED** waliomba kumilikishwa Kisheria na hivyo kuandaliwa kwa 'Allocation Letter' yenye Kumb. Na. LD/KGMC/LD/VIJ/G/10889 ya tarehe 24/03/2020.

Kidori F. Mmbaga,
**KNY; MKURUGENZI WA MANISPAA KIGAMBONI**

**Nakala:** **ELLAND ROAD LIMITED,**
S.L.P. **50071**,
**DAR ES SALAAM.**
(Fuatilia hati yako Wizara ya Ardhi).

COMMISSIONER FOR LANDS
OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENTS DEVELOPMENT
RECEIVED
DATE 14/05/2020
DAR ES SALAAM

Scanned with CamScanner